

**WAAMBIE**  
*Ninawapenda*

KUPOKEA UFUNUO

*wa Upendo wa Mungu KWAKO*

**JOYCE MEYER**

#MWANDISHI MASHUHURI KWA MUJIBU WA GAZETI LA  
*NEW YORK TIMES*

# WAAMBIE NINAwapenda

---

Ukweli Rahisi Kuhusu Upendo wa Mungu Kwako

JOYCE  
MEYER



JOYCE MEYER  
MINISTRIES

P.O. Box 5, Cape Town 8000

Unless otherwise indicated, all Scripture quotations are taken from THE AMPLIFIED BIBLE: Old Testament. Copyright © 1962, 1964 by Zondervan Publishing House (used by permission); THE KING JAMES VERSION; and from THE AMPLIFIED NEW TESTAMENT Copyright © 1958 by the Lockman Foundation (used by permission).

Copyright © 2014 by Joyce Meyer Ministries – South Africa

All rights reserved. No part of this publication may be reproduced, distributed, or transmitted in any form or by any means, or stored in a database or retrieval system, without the prior written permission of Joyce Meyer Ministries – South Africa.

Joyce Meyer Ministries – South Africa  
PO Box 5, Cape Town, 8000

Phone: +27 (0) 21 701 1056

Website: [www.joycemeyer.org](http://www.joycemeyer.org)

Go to [tv.joycemeyer.org](http://tv.joycemeyer.org) to watch Joyce's messages in a variety of languages

Tell Them I Love Them – Swahili  
Not For Resale

# YALIYOMO



<i>Utan<u>gulizi</u></i>	5
1. Mungu Anakupenda!	7
2. Je! Mimi ni Mwema vy-a Kutosha?	13
3. Upendo ni Uhusiano	19
4. Upendo, Tumaini na Imani	25
5. Uhuru Kutoka kwa Hofu	31
6. Upendo Hufikia Wengine	37
7. Upendo wa Mungu Utakubadilisha Pata Uzoefu wa Maisha Mapya	41
Ombi kwa Ajili ya Kuokoka	46



# UTANGULIZI



Ninaamini kwamba kile watu wanachohitaji zaidi ya kitu kingine chochote ni ufunuo wa kibinafsi wa upendo wa Mungu kwao. Ni kuelewa huku kunaotupatia msingi wa uhusiano wa karibu wa kindani, na wa kibinafsi naye pamoja na maisha ya Kikristo ya ushindi wa kweli. Hatuhitaji “ufahamu wa kimawazo” kuhusu upendo wa Mungu; tunahitaji ufunuo wa upendo wake miyoni mwetu. Ni Roho Mtakatifu peke yake anayeweza kutupatia ufunuo huu, na atafanya hivyo tunapoutafakari upendo wa Mungu, tunapoutambua maishani mwetu, na kuutafuta ufunuo huo kupitia kwa maandiko na maombi.

Kukubali kwamba Mungu anaupenda ulimwengu wote kiasi cha kumtuma Yesu afe kwa ajili ya dhambi za kila mmoja si jambo gumu. Lakini inaweza kuwa vigumu zaidi kuamini kwamba Mungu anakupenda sana kiasi kwamba angemtuma Yesu afe kwa ajili yako peke yako kama ni wewe tu ungelikuwa unaishi duniani.

Baada ya miaka mingi ya kuwa Mkristo asiye na ushindi wala kutosheleka, nilikuja mwishowe kupokea ufunuo wa upendo wa Mungu kwangu. Kwa neema yake, Mungu alinifunulia, kupitia kwa Roho Mtakatifu, upendo wake kwangu kwa njia ya kibinafsi kabisa. Ufunuo huo mmoja umeyabadilisha maisha yangu yote pamoja na uhusiano wangu na Yeye.

Ombi langu ni kwamba, unapokisoma kitabu hiki, utapokea ufunuo wa upendo wa Mungu kwako kama mtu binafsi. Nakutia moyo ukisome pole pole, ukitumie kama mwongozo wa kusoma zaidi

## WAAMBIE NINAWAPENDA

---

kuhusu upendo wa Mungu kwenye Biblia, na kuyatafakari maandiko na mawazo utakayoyapata kwenye kurasa zinazofuata.

Mungu anakupenda sana! Na anataka ujue na upate uzoefu wa upendo wake kila siku, katika kila sehemu ya maisha yako, jinsi tu alivyonifanya mimi. Kwa hivyo sasa nakitoa kitabu hiki kwako kwa unyenyekevu, nikijua kwamba mimi si kitu bila Mungu, na ufunuo wowote na kuelewa niliko nako kwa Neno lake ni kwa neema Yake peke yake.

# 1



## MUNGU ANAKUPENDA!

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”*

- YOHANA 3:16 UNION

Mungu anataka kuwa na jamii, na anataka kuwa Baba yetu. Tuliumbwaa kuwa na uhusiano naye na kuwa wana na binti zake, wanaoishi katika utele wa maisha ambayo Yesu alikufa kutupatia. Hii inamaanisha anataka tumtegemee, tumuegemee, tumpende, na kumkubalia atupende. Anataka tumwamini na kumtafuta kwa kwenda kwake tunapokuwa na mahitaji. Anataka kuwa na uhusiano wa kibinafsi na kila mmoja wetu.

Wengi wetu hulifirkiria andiko hili – Yohana 3:16 – kwa njia pana isivyofaa. “Ah, ndio, ninajua Yesu aliufia ulimwengu,” tunasema, lakini “ulimwengu” si kundi lisiloeleweka vizuri la watu aliowafia Yesu. Alikufa kwa ajili ya kila mmoja wetu. Alikufa kwa ajili yako!

Ukweli ni kwamba, kama ungalikuwa ni wewe peke yako uliyekuwa hapa duniani, Yesu bado angalikufa kwa ajili yako. Angeyapitia machungu yote aliyoavumilia kwa ajili yako. Mungu anakupenda ajabu, na upendo wake ni wa milele (tazama Yeremia 31:3).

Siku moja nilipokuwa nikiendesha gari langu, Mungu alinena na moyo wangu na kusema, “Joyce, wewe ni mboni ya jicho langu.” Naye adui akaifuata sauti ya Mungu unyo unyo na kusema, “Naam, na hicho si ni kiburi tele? Unafikiri wewe ni nani?” Shtaka hilo lilinifanya nikawaza, Oh, haifai niwe nikifikiri hivyo.

Kutambua kwamba sisi ni watu wa kipekee, na kwamba tunavyo vipawa vya ajabu, pamoja na talanta na uweza wa ajabu, kwa kawaida huenda kinyume na namna asili ya jinsi tunavyojifikiria. Lakini ukweli ni kwamba kila mmoja wetu ni mtu binafsi, aliyeumbwa kwa njia ya kipekee na Baba yetu. Mungu anapenda utofauti, na aliquumba uwe wa kipekee, fafanusi yake ikiwa ni kwamba hataki ujillinganishe na wengine au kujaribu kuwa kama wao. Wewe u maalum kwake jinsi tu alivyokumba!

Nilipokuwa nikifikiria juu ya kile Mungu alichokuwa amenena kwa moyo wangu, nilijipigia picha mawazoni ya mama aliye kwenye duka kuu la kununua vyakula na mahitaji mengine ya nyumbani, akiwa amesimama kando kando ya fungu la matufaha. Akayaangalia matufaha hayo yote kisha akajichagulia lile lililo kuwa bora kabisa kwake. Niliduelewa ujumbe wake Mungu kumaanisha kwamba mimi nilikuwa kama “tufaha” lililokuwa bora kabisa kwake. Mimi ndiye niliyekuwa maalum kwake. Mtizamo huo hauonekani kuwa sahihi, lakini wajua Mungu humtazama kila mmoja wetu vivyo hivyo. Si kwamba anasema wewe ni mtu spesheli kwake zaidi ya watu wengine, na wengine wote hawafai. Anasema tu kwamba sote tu spesheli kwake. Mungu anasema hivi kwa Neno lake, na Neno lake ni kwa kila mmoja wetu. Wewe ni mboni ya jicho lake.

Wakati Mungu aliponizungumzia hivi, sikulikumbatia alilokuwa anajaribu kuniambia kwa sababu nilihisi kwamba ilikuwa makosa kufikiri mawazo mazuri hivi kujihusu. Lakini baada ya siku mbili hivi, nilifungua Biblia yangu katika Zaburi 17:8, na hapo nikajipata

ana kwa ana na ukweli huu: “Unilinde kama mboni ya jicho; unifiche chini ya uvuli wa mbawa zako. “Nikasema, “Jamani! Hakika ni Mungu aliyenizungumzia. Mimi ni mboni ya jicho lake.” Ilinifanya nijisikie mtu spesheli kila nilipofikiri juu ya jambo hili. Je, wajua kwamba wewe ni wa thamana kuu sana kwake Mungu, na anataka ujihisi spesheli, wa kuthaminiwa, ghali na aliyependwa?

Watu huwa na tamaa kuu miyoni mwao ya kupendwa. Mungu alituumba hivyo. Watu wengi huamini kwamba Mungu anaupenda ulimwengu na kwamba anampenda Yesu, lakini wana wakati mgumu kuamini kwamba Mungu anawapenda wao kama watu binafsi. Lakini Neno linafundisha kwamba Mungu anatupenda jinsi anavyompenda Yesu. Yohana 3:16 inatuonyesha hivi. Naye anataka kumimina upendo na baraka zake maishani mwetu jinsi tu anavyompenda na kumbariki Yesu. Yohana 5:20 inasema, “Baba anampenda Mwanaye kwa njia kuu na anamfunulia (kumwonyesha) kila kitu anachokifanya Yeye. Na atamdhahirishia (kumruhusu aone) mambo makuu zaidi kuliko haya, ili mweze kushangaa na kustabajabu na kupigwa na butwaa.” (Tafsiri ya AMPLIFIED)

Mungu anasema hapa, “Ninayafanya makuu haya yote kuitia kwake Yesu, na nitafanya hata makuu zaidi ya haya kuitia kwa Yesu, ili mshangae” (fasiri yangu). Mungu anataka kutustaajabisha kwa kufanya mambo makuu kwa ajili ya kutuletea mema na furaha tele.

Huwa tunayasoma maandiko haya, lakini mara nyingi huwa tunakosa kuelewa si kile ambacho Mungu anataka kutufanyia tu, bali pia na hasa kile anachotaka kufanya kuitia kwetu. Katika Yohana 14:12, Yesu anasema, “Amin, amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.”

Mungu huwafanyia watu vitu vingi kila siku kwa sababu

anawapenda, lakini wanakosa kuviona vyote awafanyiavyo. Litafakari hili, kwa mfano: Jua linapochomoza kila siku, linachomoza kwa ajili yako wewe na mimi. Maua huchanua kwa njia nyingi tofauti, zote kwa ajili ya kutupendeza na kutuletea furaha. Ulimwengu aliotuumbia Mungu ni wa kupendeza ajabu, na anataka tuufurahie! Sura ya 1 katika kitabu cha Mwanzo inasema kwamba Mungu alimpa mwanadamu mamlaka na kumwambia azitumie rasilimali zote za dunia kumhudumia Mungu na mwanadamu mwenzake.

Mvua ijapo katika majira yake, inanyesha kwa ajili yako. Theluji ijapo, inakuja kwa ajili yako. Hatua zako zimeongozwa na Bwana, na wakati wote anakutazama wewe.

Kumbukumbu la Torati 7:9 inasema, “Basi jua, tambua na uelewe kwamba Bwana Mungu wako, Yeye ni Mungu, Mungu mwaminifu, anayeweka agano lake na upendo wake usiokoma na rehema zake kwa wale wampendao na kuzishika amri zake, hata kwa vizazi elfu moja.” (Tafsiri ya AMPLIFIED)

Upendo wa Mungu kwetu ni wa milele na usio na masharti. Wengi wetu hufikiria tumemchosha na kushindwa kwetu na makosa yetu, lakini hatuwezi kufanya hivyo. Na haijalishi utafanya nini, huwezi kumfanya Mungu akome kukupenda. Upendo si tendo analolifanya Mungu, upendo ni kile alichoso.

Ukifikiri kwamba wewe ndiwe mtu yule mmoja mwovu kabisa asiyeweza kupendwa na Mungu, umekosea. Hakuna tundu lililo la kina kikuu sana kiasi kwamba Mungu hawezikukufikia na kukuinua. Ana mpango wa kuleta urejesho kwako. Si kwamba atakusamehe dhambi zako tu ukimwomba kwa uaminifu kufanya hivyo, pia atazisahau na kuziweka mbali nawe jinsi mashariki ilivyo mbali na magharibi (tazama Zaburi 103: 10-12). Unaweza kusema, “Nilimpokea Yesu moyoni mwangu, na ninampenda.” Lakini nami nakuuliza, unaamini

kiasi gani kwamba Mungu anakupenda?

Upendo wa Mungu usiokoma, usio na masharti ni ujumbe rahisi, lakini pia ndio msingi halisi ambao ni lazima auweke maishani mwako ili uweze kuelewa kila kitu kingine alicho nacho kwako. Ninaamini ndio mwanzo wa uponyaji wote maishani mwetu. Hailijalishi ni kipi kingine utajifundisha, wala jinsi utakavyojibidiisha kusoma na kutafuta mambo ya Mungu, ikiwa huwezi kukubali kwamba anakupenda bure na kwa ukarimu mkuu, hutapiga hatua za kwenda mbele kwa kiwango kikuu katika kutembea kwako naye. Huwa tunapokea kutoka kwa Mungu kwa imani, lakini hata imani hufanya kazi kupitia kwa upendo (tazama Wagalatia 5:6). Kwa hivyo tusipopokea upendo wa Mungu, hatuwezi kupokea chochote kingine.

Upendo wa Mungu pia hutuwezesha kuishi bila hofu (tazama 1 Yohana 4:18), jambo muhimu katika kufurahia maisha na kuitimiza hatima yetu. Je, utapokea bure upendo wake kwako? Sio wa kuuzwa; huwezi kuununua kwa kufanya matendo mazuri...kile tu unachowenza kufanya ni kuupokea, kuupokea na kupokea.



# 2



## JE! MIMI NI MWEMA VYA KUTOSHA?

*“Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi. Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenyе dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake.”*

- WARUMA 5:5-10

Ni rahisi kuamini kwamba Mungu hutupenda bora tusitende kosa. Shida ya mtizamo huu ni kwamba watu wengi hawajipendi, na hii huwafanya kuhisi kwamba huenda hata Mungu hawapendi sana. Lakini Biblia inasema, “Mtu ni kitu gani hata umkumbuke?” (Zaburi 8:4). Sisi ni viumbe vya Mungu, na kuusema ukweli huu kwa urahisi, anatupenda kwa sababu anatupenda. Yeye ni upendo (tazama 1 Yohana 4:16). Mungu anatupenda kwa sababu anataka kutupenda!

Anakupenda, na wewe ni mtu maalum kwake. Hiyo inamaanisha

wewe ni mtu tofauti na wa kipekee. Hufai kuwa jinsi nilivyo, na sifai kuwa jinsi ulivyo. Na utajawa huzuni tele maishani mwako ukishinda ukijaribu kujilinganisha na wengine na kushindana nao. Matokeo ya kufanya hivyo ni kumpa adui nafasi ya kukuambia kwamba wewe sio mwema nya kutosha. Ukweli ni kwamba, ukiwa pamoja na Mungu, si lazima uwe “mwema nya kutosha.” Yesu ameshakuwa “mwema nya kutosha” kwa niaba yako. Alizilipia dhambi zako na kuchukua adhabu uliyostahili kupata.

Biblia inasema kwamba kama alikupenda nya kutosha kufa kwa ajili yako, basi anakupenda kwa kiasi gani sasa wakati umefanywa haki kupitia kwa damu yake? (tazama Warumi 5:8-9). Bila shaka anakupenda nya kutosha kufunika makosa yako ya kila siku na kukuweka safi kutoka kwa udhalimu wote.

Huu ni mfano wa jinsi ninavyofikiria Mungu huyatazama makosa yetu na kupungukiwa kwetu. Mfikirie mtoto mdogo, wa umri wa miaka mitatu au minne, ambaye kila wakati anamtazama mama yake akifanya kazi ya nyumbani mwao. Anampenda mamake sana, kiasi kwamba anajitafutia ndoo ndogo ya maji na kakitambaa kadogo, kisha anaenda kwenye dirisha iliyo upande wa mlango wa mbele. Anaisugua dirisha ile vyema kabisa, kisha anatafuta karatasi za kuipanguza dirisha ile na kuikausha.

Bila shaka, dirisha ile inabaki na mistari na povu la sabuni, licha ya kwamba kale kasichana kalitumia kitambaa kile kizuri kabisa akitumiacho mama kusafisha. Lakini yule mtoto anaingia ndani na kwa sauti yake nzuri ya kitoto na ya kuvutia anasema, “Mama, Mama, nilikuoshea dirisha yako! Nilikufanya kazi nzuri sana. Nakupenda Mama!”

Yule mama aliyejawa na upendo anasema, “Ah, hilo ni jambo jema ajabu ulilolifanya! Ahsante kwa kunisiaidia.” Kisha, punde tu mtoto anapoendelea kushughulika mahali pengine, anaisafisha dirisha ile. Baadaye, anamtia moyo binti wake kuomba usaidizi ili

aweze kujifundisha jinsi ya kuifanya kazi ile kwa njia inayofaa.

Hivi ndivyo Mungu anavyotufanya. Na anaweza kufanya kazi pamoja nasi katika mambo yote ili kutuletea mema kama tunampenda na kuitwa kwa kusudi lake (tazama Warumi 8:28). Ikiwa unafanya bora kabisa kulingana na kile unachoju, hicho ndicho Mungu anachotarajia kutoka kwako. Anaweza, na hakika atakusaidia kupiga hatua mbele ukiendelea kumtafuta. Atakubadilisha umfanane kutoka utukufu hadi utukufu (tazama 2 Wakorintho 3:18).

*“Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo! Baba ampenda Mwana, naye amempa vyote mkononi mwake”* (Yohana 3:34-35).

Siku moja nikiwa ninaisoma aya hii kwa undani, nililia machozi nilipogundua kwamba Mungu hatupatii Roho wake kwa kipimo. Hatupatii kionjo kidogo cha hili na kionjo kidogo cha lile. Yeye ni mkarimu na anaweza kuyafanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo! (tazama Waefeso 3:20).

Katika Kumbukumbu la Torati 7:6-7, Mungu anasema, “Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa BWANA, Mungu wako; BWANA Mungu wako amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. BWANA hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote.”

Hilo ni jambo la kusimkia. Mungu anasema, “Niliamua kukupenda, na nikakwambia kwamba u mtakatifu. Nikakwambia kwamba wewe ni wa kipekee. Nilikuchagua, si kwa sababu wewe ni mwema kwa nguvu zako mwenyewe, lakini kwa sababu ninakupenda.” Unajua ni nini Mungu anataka ufanye leo? Anataka uukubali upendo wake. Wacha kumwambia Mungu makosa yako yote na kila kitu kisichofaa ndani yako; maana hata hali iwe jinsi ilivyo si kwamba hakutarajia kumpata mtu kama wewe. Tayari alikuwa anajua kila

kitu kukuhusu, ikiwa ni pamoja na kila kosa utakalowahi kufanya alipokuvuta kwake ili kuwa na uhusiano nawe.

Shida kubwa kabisa ya wengi wetu ni kwamba hatujipendi. Na kwa sababu hiyo, hatuamini Mungu anatupenda, au kwamba kuna yejote anayetupenda. Kwa hivyo tunafikiri, “Yawezekanaje tupendwe na yejote? Mimi ni mtu mwenye shida tele!” Na ukiamini kwamba wewe ni mtu mbaya kupindukia, basi huenda matendo yako yataambatana na yale ya mtu mbaya kupindukia. Ukweli ni kwamba, huwezi kuinuka juu ya picha ya jinsi unavyojiona moyoni mwako.

Shida kubwa kabisa niliyokuwa nayo ilikuwa ni kwamba sikujipenda, na nilitumia muda wangu mwingi nikijaribu kujibadilisha kuwa yule ambaye nilifikiria nilistahili kuwa. Kwa mfano, nilifikiri kwamba nilikuwa mtu wa kupiga domo kupita kiasi, hivyo nilikuwa nikijaribu kuwa mnyamavu. Lakini nilipokuwa nimenyamaza, nilipata kwamba nilikuwa ninahuzunika na kukosa furaha, na kila mtu aliyejikuwa karibu nami alikuwa akitaka kujua ni kwa nini nimenyamaza. Kisha ningeanza kufikiri, “Mliniambia kwamba mimi ni mpiga-domo kupindukia, na ninajaribu nisiongee sana. Basi niacheni nilivyo!”

Siwezi kukuambia ni miaka mingapi nilipitia hali kama hizi huku nikiendelea kujipata taabani kwa sababu ya mdomo wangu kwa sababu nilikuwa nikijaribu kujibadilisha. Na shetani daima alikuwa tayari kuniambia jinsi niliyokuwa mwovu kila wakati jambo kama hili lilipotokea kwa sababu yeje hufanya kazi usiku na mchana kutufanya tujihisi wenye hatia na waliohukumiwa. Kwa hivyo ninaelewa jinsi inavyoweza kuwa changamoto kuamini kwamba Mungu angali bado anakupenda hata wakati umekosea.

Mungu anataka uwe huru kutoka kwa hukumu ya adhabu na kujihisi mwenye hatia, lakini unahitaji imani na ujasiri ili kuwa huru. Je! Wajua kwamba hakuna kiasi wala kina cha kujihisi mwenye hatia kinachoweza kulipia hata kosa moja ulilolifanya au utakalolifanya?

Nataka kuirudia kauli hii: Kuamini kwamba Mungu anakupenda wakati umekosea inaweza kuwa ni changamoto kuu.

Shetani atajaribu kukuchukiza na mawazo kuhusu jinsi ulivyo mbaya. “Angalia ulichokifanya sasa,” atasema. “Unafikiri wewe ni nani? Mungu hatakubariki kamwe...ungejithahidi ufanye afadhali kuliko hivi. Huwezi kumwambia yejote kumhusu Yesu sasa. Mungu hawezi kukutumia. Na hatajibu maombi yako. Huwezi kufanya chochote chema wala kwa njia ifaayo.”

Hapo ndipo unapohitaji imani katika Mungu na ujasiri wa kuinuka na kusema, “Baba, nilikosea, nakuomba unisamehe. Ninajuta kwa moyo wangu wote kwa kile nilichokifanya, na ninataka msamaha wako.” Ni vizuri pia kumjibu shetani. Mkumbushe kwamba Yesu alikwisha zilipia dhambi zako na tayari umesamehewa na kuwekwa huru toka kwa hukumu ya adhabu na hisia za kuwa na hatia. Nguvu za Neno la Mungu zikifanya kazi maishani mwako zitajengwa imani yako na tumaini lako katika yeye. Kisha utaweza kuyafurahia maisha yako na kuwa baraka kwa wengine!

Unaweza kuwa ukifikiria, Mbona ninashinda nikilirudia kosa lile potovu tena na tena na tena? Nilikuwa nikifikiri hivyo pia, mpaka nikaamua kutokubali hukumu ya adhabu kuhusu jambo hilo iendelee kuwa juu yangu tena. Utakapoamua kuacha kuishi na hukumu ya adhabu na hisia za kuwa mwenye hatia, itakusaidia kuacha kilitenda kosa hilo.

Hisia za hatia na hukumu ya adhabu hukushusha moyo na kukufinyilia chini kiasi kwamba huwezi kuwa huru. Inakufanya unadhoofika na kupungukiwa na nguvu na inakuwa ni rahisi kuendelea kuanguka dhambini. Hii ndio sababu ni lazima uwe jasiri kuhusu kupokea karama ya Mungu ya msamaha na kuipinga hukumu ya adhabu. Lazima uchague kuishi kwa imani kuhusu kile ambacho Mungu amesema katika Neno lake na kukataa kugaagaa kwenye tope la kujihisi mwenye hatia. Adui bado atakwambia, “Yaani unamaanisha

kwamba hutahisi vibaya kuhusu kosa hilo? Yafaa usononeke angalau kwa masaa machache. Hicho ni kitu kibaya sana ulichokifanya.” Lakini kile tu unachohitajika kusema ni hiki, “La, sitafanya hivyo. Sitalisononekea jambo hilo hata kidogo.” Kisha umwombe Mungu akusaidie na akupe neema ya kuitikisa hisia hiyo ikuondokee na uendelee kupiga hatua za kwenda mbele. Mara za mwanzo mwanzo utakapofanya hivi itakuwa vigumu kwako, lakini itaendelea kuwa rahisi zaidi na zaidi.

Katika Isaya 53, tunasoma kwamba Yesu alipozichukua dhambi zetu kwa ajili yetu, alijitwika pia masikitiko yetu (na hayo ni pamoja na hukumu ya adhabu). Shetani hataki uwe huru kutoka kwa hukumu ya adhabu. Kwa nini? Kwa sababu wakati umehukumika, huwezi kwa kweli kupokea upendo wa Mungu. Hukumu ya adhabu hukutenga na Mungu na huwezi kuufurahia uwepo wake. Inayatoa macho yako kutoka kwa Mungu na kuyaweka juu yako.

Unaweza kuishi huru kutoka kwa hukumu ya adhabu kwa kuamini kwamba Mungu aliposema kuwa neema yake inatosha kuzifunika dhambi zako zote, alisema akiwa amemaanisha. Anakupenda, na neema yake na msamaha wake ni karama zake za kupokelewa bure. Zipokee leo!

# 3



## UPENDO NI UHUSIANO

*“Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.”*

- 1 JOHN 4:16

Kama andiko hili lisemavyo, Mungu ni upendo, na anataka tutambue, tuwe na uzoefu pamoja na ufahamu nafsini mwetu wa upendo wake. Hivyo unawezaje kupokea ufahamu zaidi wa upendo wa Mungu nafsini mwako? Haijalishi anakupenda kiasi gani, kama huna ufahamu wa upendo wake, hautakuwa wa manufaa yoyote kwako. Fikiria unavyohisi mtu anapokuonyesha upendo mwangi. Unapojuia kwamba unapendwa, unakuwa na ujasiri. Mungu anakupenda, na anataka kukuonyesha upendo huo. Anakaribisha kila mmoja wetu awe na uhusiano wa kina, wa karibu na wa kibinafsi naye. Anataka kukaribishwa ahusike na kila kitu tunachofanya. Na anataka tuwe na mazungumzo endelevu naye, jinsi tu tungalivyokuwa nayo na rafiki wa karibu.

Je! Una uhusiano wa kweli na wa kibinafsi na Mungu? Tunapozaliwa mara ya pili, hatupokei ushirika mtamu na wa kina na Mungu moja kwa moja. Ni lazima tuukuze uhusiano wetu naye, jinsi tu tunavyofanya na mtu mwininge yejote yule.

Nilikuwa Mkristo kwa miaka mingi kabla sijamaanisha kabisa

kuhusu kutembea na Mungu. Nilikwenda kanisani kila Jumapili na hata kufanya kazi kidogo ya kujitolea pale, lakini bado nilikuwa sijamweka Mungu kati kati ya maisha yangu. Nilijisikia mtupu na asiyetosheleka. Lakini sasa, ye ye ndiye wa kwanza ninayemfikiria asubuhi na jambo la mwisho ninalolifkiria usiku. Tunakuwa na ushirika pamoja naye mchana kutwa, na hakuna jambo ninalolitamani zaidi kuliko kumtumikia Mungu wangu na kumpendeza. Kuna tundu lililo na umbo la Mungu ndani ya kila mmoja wetu – upweke amba ni Mungu peke yake awezaye kuujaza. Hakuna chochote unachoweza kutafuta au kutamani kinachoweza kuijaza sehemu hiyo ndani yako. Nakutia moyo ujiulize swalii hili: Nimemaanisha kiasi gani kuhusu uhusiano wangu na Mungu? Niko tayari kumweka ye ye na mapenzi yake mbele ya vitu vingine vyote? Ninaweza kusema kama Paulo alivyosema katika Matendo 17:28, “Ndani yake ye ye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu?”

Mungu anakupenda, na wewe ni mtu maalum kwake. Alikuumba ili uwe na uhusiano naye. Hii ndio shauku yake kuu kabisa kukuhusu, na mapenzi yake kamilifu kwa ajili ya maisha yako. Yeye hukunong’onezea moyoni mwako kila kukicha, “Habari ya asubuhi, ninakupenda.” Ikiwa umekuwa humsikii akisema hivyo kwako, je, utaanza kumsikiliza na kumwamini?

Rafiki yangu mmoja alikuwa na picha hii mawazoni mwake ya Mungu Baba akienda kwenye nyumba za watu kule Marekani walipoamka asubuhi. Aliingia mle ndani akiwa tayari kushiriki na kuongea nao. Alichukua kitimezani mwao na kukaa chini. Wale watu waliamka wakawa, wakija na kwenda, wakija na kwenda. Walikuwa wakimwambia Mungu, “Baadaye, Mungu. Kaa papo hapo ulipo kwa mda mfupi. Punde tu nikimaliza shughuli hii, nitazungumza nawe. Nitakuwa na ushirika nawe baadaye, Mungu. Baadaye, Mungu.”

Hatimaye, mwisho wa siku ulifika. Mungu akaondoka nyumbani mwao huku akionekana mwenye huzuni kwa sababu hakuna aliyejukua

kuzungumza naye siku hiyo. Kila mtu alikuwa anajishughulisha sana eti na mambo mengine muhimu kiasi kwamba hawakuwa na wakati wa kumpa Mungu.

Usiwe na shughuli nyingi sana kiasi cha kukosa mda wa kumpa Mungu. Ikiwa huna wakati wa kuomba na kuwa na ushirika naye, basi wewe ni mwenye shughuli kupindukia. Chukua mda na kumwambia Mungu jinsi unavyopenda. Kila kitu kitakapopita na kuisha, hakutakuwa na chochote kilichobaki ila Mungu peke yake! Na ikiwa kufikia wakati huo hutakuwa na uhusiano naye, utakuwa umepitwa na wakati wa kuanza na kuimarisha uhusiano naye.

Babangu mzazi aliaga dunia hivi maajuzi, na ninafurahi kuripoti kwamba alimpokea Yesu kama mwokozi wake kama miaka mitatu hivi kabla hajafa. Japo baba yangu alienda mbinguni, alikosa furaha ya kuishi maisha ya ushindi katika Mungu. Alijiishia mwenyewe wakati wote. Usifike mwishoni mwa maisha yako ukiwa umejawa na majuto ya hasara ya maisha yako kwa sababu uliyatumia kwa vitu visivyo na maaana kamwe. Wakati ni karama ya ajabu kutoka kwa Mungu, na ni muhimu tuwe waangalifu sana tunatumia wakati wetu kufanya nini. Wajua, mradi tu tumeshautumia mda, hatuwezi kuupata tena. Kuwa na wakati na Mungu huleta thawabu ya ajabu, lakini vitu vingine vingi huleta sisimko lisilo na thamani kwa bei ghali.

Ninapendekeza ufanye uamuzi wa kutumia mwaka ulio mbele yako ukitilia mkazo jambo la upendo wa Mungu, ukisoma maandiko yanayozungumzia upendo, ili ujifunze jinsi ya kupokea upendo wake. Upendo wake huleta uzima, amani, na furaha na msisimko wa kuishi. Na anataka tutulie na kufurahia kuwa mtoto wake. Soma maandiko kuhusu asili yake na upate kumfahamu vyema zaidi.

1 Yohana 4:16 inasema, “Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi na kuliamini.”

Huenda usijihisi aliyependwa asubuhi na mapema uamkapo.

Labda huna nguvu hata kidogo, na unaona jinsi itakavyokuwa rahisi kuwa na manung'uniko mchana kutwa. Habari njema ni kwamba, unaweza kubadilisha nia yako kwa kuzungumza maneno ya kutia moyo na imani. Tamka kwa sauti, "Mungu ananipenda sana. Mimi ni mboni ya jicho lake, na ana mpango mwema kwa ajili yangu." Ukizungumza juu ya Mungu na Neno lake badala ya shida zako na hisia zako, unaweza kuleta tofauti kwa siku yako yote.

Lazima ujizungumzie na umakinike kwamba umezungukwa na upendo wa Mungu. Biblia inasema kwamba Mungu amechora piche yako katika vitanga vya mikono yake (tazama Isaya 49:16). Ninaweza kumwona kule juu akisema, "Tazama, unaona hapa? Ah, jamani, si wanapendeza? Ninawapenda sana. Ona watoto wangu, papa hapa kwenye vitanga vya mikono yangu." Amekuweka hapo kama kumbukumbu daima kwamba anakupenda na anatamani ushirika na wewe.

Kumbuka kuwa mtu wa shukrani daima kwake Mungu na kukuza uhusiano wa ushirika endelevu naye. Nyakati zingine huenda utaamua kuacha shughuli zako zote na kuchukua mda mfupi na kumshukuru Mungu kwamba unamjua na kumwambia jinsi alivyo wa ajabu. Tulia na umpende Mungu. 1 Yohana 4:16-17 inasema, "Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu."

Kufahamu kwamba Mungu anakupenda hukupa ujasiri wa kumwamini na kuutumainia uaminifu wake. Baraka zote alizo nazo kwa ajili yako zitakufikia kwa kumruhusu Mungu akupende: imani kuu zaidi, ushindi juu ya dhambi, amani moyoni mwako, uponyaji, maisha yaliyojaa utele wa karama zake na furaha. Na zinaweza kukufikia tu kwa kumruhusu Mungu akupende. Mara nyingi huwa tunaugeuza ukweli huu na kufikiri, "Naam, lazima nimpende Mungu." Ninaamini kwanza lazima umruhusu Mungu akupende. Siamini unaweza kumwonyesha Mungu upendo wako mpaka umruhusu

akupende kwanza. Biblia inasema kwamba tunampenda kwa sababu alitupenda kwanza (tazama 1 Yohana 4:19).

Tunapojuja kwamba Mungu anatupenda na kuupokea upendo wake, hapo ndipo nasi tunaweza kumpenda pia. Tunaweza kuwa na ushirika naye. Unaweza kuwa unajiuliza, unawezaje kuwa na ushirika na Mungu? Mungu aliponiambia niwe na ushirika naye, niliketi tu kwenye kiti changu cha kupumzika na kusema, “Nifanye nini sasa, Mungu?” Kweli kabisa! Sikujua jinsi ya kuwa na ushirika na Mungu kwa sababu, wakati huo, sikujua kwa kweli jinsi alivyokuwa ananipenda, na sikuwa nimeelewa kwamba anataka niwe rafiki yake na mwandani wake wakati wote. Nilipoendelea kuwa na wakati naye, nikiomba, nikilisoma Neno na wakati mwingine kukimya tu uweponi mwake, nilijifundisha jinsi ya kufurahia ushirika na Mungu.

Ninataka nikutie moyo uchukue hatua ya kwanza. Mpe Mungu nafasi, naye atakufundisha jinsi ya kuwa na ushirika naye. Sitajaribu kukupatia aina yoyote ya utaratibu wa namna ya kuwa na ushirika na Mungu. Sitaki eti uwe na hatua ya kwanza, ya pili, ya tatu, na kadhalika. Ningependa uongozwe na Roho wake Mtakatifu. Mungu anataka ustarehe unapokuwa pamoja naye ... maana si ni kweli kwamba, kulingana na Waefeso 3:17, moyo wako ni nyumbani mwake Kristo?



# 4



## UPENDO, TUMAINI NA IMANI

*“Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo.”*

- WAGALATIA 5:6

Wengi wetu hutumia mda mwingu sana katika jitihada za kujaribu kuwa na imani. Tunajua kwamba bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu (tazama Waebrania 11:6), kwa hivyo tunatia bidii na kukazana kuwa na imani zaidi. Lakini imani hukua moyoni mwetu, na tunaipata tu kupitia kwa uhusiano unaopenda ushirika wa upendo wa Mungu na kulisikia Neno lake. Huwa inakuja tu kupitia kwa ufunuo utokao kwa Mungu. Ama kwa kweli, siwezi kukufundisha imani, lakini ninaweza kukufundisha kanuni za imani na kukutia njaa ya kuipokea sana kiasi kwamba utafanya chochote kuipata. Imani ni mkono ule unaonyoshwa kwake Mungu na kupokea kutoka kwake.

Tunahitaji kuacha kung’ang’ana sana katika jitihada za kupata imani ili kumpendeza Mungu, na kuanza kutumia mda huo wote na bidii hiyo yote kuwa na Mungu, tukimpenda na kupokea upendo wake. 2 Wakorintho 5:7 inasema, “Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona.” Wakati mmoja nilipokuwa nikilisoma andiko hili, nilihisi Mungu akinena mambo yaliyokuwa na nguvu za kunipeleka mbele moyoni mwangu. Alinionyesha kwamba si kutaka na kujaribu kwangu kutembea kwa imani kunaoleta mabadiliko. Aya hii inasema kwamba nitaweza tu kutembea kwa imani kulingana na

kile ninachoamini kuhusu uhusiano wangu na Mungu. Hebu tulia na ulifikirie hilo. Jiulize unahisi nini kuhusu uhusiano wako na Mungu. Mtu anayeamini kwamba yeche si mwenye haki machoni mwa Mungu hawezi kutarajia kutembea kwa imani. Tumefanywa wenyewe haki mbele za Mungu kupitia kwa dhabihu yake Yesu Kristo (tazama 2 Wakorintho 5:21). Haki yetu mbele zake haina msingi wake juu ya kile tulichofanya au tutakachofanya; msingi wake ni kile Yesu alichofanya. Kwa hivyo mtu anayeamini kwamba yeche ni mwovu aliyeshindwa, na kwamba Mungu hampendi, hawezi kutembea kwa imani.

Wagalatia 5:6 inasema kwamba imani hutenda kazi kupitia kwa upendo. Watu wengi hufikiria kwamba andiko hilo humaanisha kwamba ikiwa wataweza kuwapenda watu wengine, basi imani yao itafanya kazi kwa ajili yao na hapo wataweza kupokea wanachohitaji kutoka kwa Mungu. Japo ni kweli kwamba Mungu anataka tutembee katika upendo, haiwezekani kufanya hivyo mpaka kwanza tumruhusu atupende. Ni rahisi sana: hatuwezi kuwapa wengine kile tusichokuwa nacho. Nilijaribu miaka mingi kutembea katika kuwapenda watu kwa sababu nilijua ilikuwa ni amri ya Mungu, lakini mara tena na tena nilishindwa hadi nilipoupokea upendo wa Mungu usio na masharti. Jinsi nilivyoendelea kupata na kuwa na hisia nzuri kujihusu ndivyo nilivyoweza kuwafikia wengine na upendo wa kweli. Unapopata kujua kwa kweli kiasi cha upendo wa Mungu kwako, itakuwa rahisi zaidi kwako kupokea kutoka kwa Mungu na kuona mahitaji yako yakinimizwa naye. Sababu ambayo huwafanya watu wengi wasipokee ni kwamba hawaamini kwa kweli, kikamilifu, kwamba Mungu anawapenda na anataka kukutana na mahitaji yao na kuwabariki.

Unaweza kusema, “Ningependa kuamini hivyo, lakini ni vipi nitafanya hivyo?” Upendo wa Mungu uko ndani yako, na kile tu unachohitaji kufanya ni kuanza kuutambua anapokuonyesha. Biblia inasema, “Tunampenda kwa sababu alitupenda kwanza” (1 Yohana 4:19). Haingewezekana kabisa kumpenda Mungu kama hungekuwa

na uhakika kwamba Yeye anakupenda kwanza.

Upendo wa Mungu u moyoni mwako...ndani kabisa, kilindini mwa moyo wako. Na utaufahamu ukweli huu utakapoanza kujiona jinsi anavyokuona. Anasema wewe ni wa ajabu, mrembo, mwenye umbo na sura nzuri, aliyetunukiwa talanta za ajabu na wa thamani kwake. Mungu anakupenda. Hakuna yeyote ulimwenguni atakayewahi kukupenda jinsi Mungu anavyokupenda. Kadri unavyozidi kutafakari juu ya upendo wa Mungu, ndivyo utakavyoweza kuiachilia imani yako zaidi na kuishi maisha aliyoyakusudia uishi.

Huhitaji yejote bali Mungu, lakini atawaweka watu wengine maishani mwako. Ukweli ni kwamba kama hakungekuwa na mtu mwingine ila wewe na Mungu tu, bado maisha yako yangeendelea sawa tu. Mungu atakuwa rafiki yako wa karibu zaidi. Atakuwa mwenza wako ikiwa huna mwenza. Atakuwa baba au mama ambaye huenda huna. Yeye ndiye kila kitu unachohitaji. Usifanye kosa lile la kumwomba Mungu akufanyie vitu tu; mwombe akupe uwepo wa nafsi yake zaidi maishani mwako. Mwombe ajaze nafsi yako na utele wa nafsi yake Mwenyewe (tazama Waefeso 3:16, 19).

Mungu anakupenda na anataka kukutana na mahitaji yako na kutimiza matamanio ya moyo wako. Bora tu ujifurahishe katika Yeye, atakupatia vitu hivyo kwa njia yake mwenyewe na katika wakati wake (tazama Zaburi 37:4). Mungu alimwambia Ibrahimu kwamba atambariki na kumfanya baraka kwa wengine. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka kukufanya, lakini lazima uamini hivyo! Achilia imani yako na uziamini ahadi zote za Mungu, kwa sababu zimetolewa kwa ajili yako!

### **Imani Dhidi ya Kazi za Mwili**

Waefeso 2:8 inasema, “Kwa maana mmeokolewa kwa neema (kibali cha Mungu msichokistahili).” Je! Unatambua kwamba hukufanya chochote ili kupokea wokovu? Wengine wetu walikuwa wenye

dhambi waovu kweli kweli Yesu alipotuokoa, na karama yake ya wokovu kwa hakika haikuwa kwa sababu ya uwezo wetu wa kufanya chochote chema. Ilikuwa ni kwa sababu ya kitu kimoja tu: Mungu alitupenda sana hata akamtoa mwanawewe wa pekee ili ye yote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele (tazama Yohana 3:16).

Fafanusi mojawapo ya neno neema ni kwamba ni tamaa aliyo nayo Mungu kutumia nguvu zake maishani mwako kukutana na mahitaji yako. Jinsi tu Mungu, kwa neema, alikupatia imani tosha ya kupokea wokovu, vivyo hivyo, kwa sababu ya upendo wake anakupatia imani unayohitaji ili kuamini na kupokea vitu vingine unavyotaka au unavyohitaji. Waweza kuwa unataka wapendwa wako – wale walio katika familia yako – kumpokea Kristo, lakini ukweli ni kwamba huwezi kumfanya ye yote ampende Mungu. Unaweza kuomba na kumuuliza Mungu afanye kazi miyoni mwao, lakini huwezi kufanya itendeke kwa nguvu na kazi yako mwenyewe.

Kazi za mwili, au vitu tunavyojaribu kufanya kwa nguvu zetu wenyewe daima hutuwacha tukiwa na hisia za usumbufu wa kushindwa kwa sababu tunajaribu kufanya kitu ambacho ni Mungu pekee anayeweza kukifanya. Unakuta kwamba tunafanya kazi na hatupati matokeo mazuri hata kidogo. Tunachohitajika kufanya ni kunyenyeka mbele za Mungu na kumwomba atupe msaada wake. Biblia inasema katika 1 Petro 5:5 kwamba Mungu mwenyewe hupinga, huzuia na kuwashinda wenyewe kiburi, lakini huwapa “neema (kibali, baraka) wanyenyekuvu.”

Neema ya Mungu ni muhimu sana maishani mwetu. Tuliokolewa kwa neema kupitia kwa imani, na vile tulivyookolewa ndivyo tunavyofaa kuishi kila siku ya maisha yetu – kwa neema ya Mungu kupitia kwa imani. Ukishakuwa na msingi huu wa upendo wa Mungu maishani mwako, hapo ndipo utakapoanza kumwamini na kuwa na tumaini lako ndani yake. Utaweza kutembea kwa imani na si kwa kuona. Utajua na kuwa na uhakika moyoni mwako kwamba Mungu

ni mwaminifu katika kutimiza ahadi zake.

Kulingana na tafsiri moja ya Biblia ya Kiingereza iitwayo “THE AMPLIFIED BIBLE”, imani ni kule kuegemea kikamilifu kwa haiba ya mwanadamu juu ya Mungu, kwa tumaini lisilo na shaka yoyote pamoja na kuwa na ujasiri kuhusu nguvu, hekima na uzuri wake” (Wakolossai 1:4). Unapomruhusu Mungu akupende, utawenza kufanya hivyo. Kadri uhusiano wako na Mungu unavyokuwa wa kina zaidi, ndivyo na imani yako inavyozidi kukua pia. Utaona Mungu akifanya mambo makuu ndani yako na kupitia kwako, na kwa ajili yako pia, lakini yote hayo yanaanza na kuwa na ufunuo wa upendo wake. Mungu anukupenda! Usiwe na wasiwasi yoyote kuhusu ukweli huo.



# 5



## UHURU KUTOKA KWA HOFU

*“Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.”*

- 1 YOHANA 1 4:18

Tunaweza kufika mahali maishani mwetu ambapo tunaendelea vyema tu katika imani, huku tukiwa na tumaini letu ndani ya Mungu na kuwa na ujasiri kwamba anatupenda. Kisha ghafla, adui anatuma kitu cha kutushambulia. Mazingira ya maisha yetu – yaani yale mabaya yanayotutendekea – yanaweza kuijaribu imani yetu kwa njia ambayo jambo jingine halingeweza kuijaribu. Watu wengine hawana shida kuamini kwamba Mungu anawapenda mpaka wakati ambapo hali pingamizi inainuka maishani na kuijanya ionekane kana kwamba hatupendi.

Hapo ndipo adui hukuingilia na hofu na hukumu ya adhabu ili kukutenga na kitu kile kile kinachoweza kukusaidia – upendo wa Mungu. “Naam, ni vipi kwamba hili limetokea kwako?” adui husema. “Nilifikiria Mungu anakupenda. Ikiwa anakupenda, basi ni kwa nini mambo mabaya yanakutendekea? Lazima ulifanya kitu kibaya ajabu. Mungu amegadhabika na wewe vibaya.”

Katika nyakati hizi za majaribu na machukizo, zinazoonekana

kuwa nyakati za kuonewa na kutendewa isivyofaa, ni rahisi kupoteza matumaini yako katika Mungu. Si kila wakati Mungu huwa anafanya mambo vile au wakati ule tunaofiki anaafaa kuyafanya. Ana mpango mkuu zaidi kuliko wetu. Anataka kutubadilisha, zaidi ya vile anavyotaka kubadilisha hali za maisha yetu. Na mara nyingi ye ye hutumia hali chungu tunazozipitia kuijenga imani yetu ndani yake na kutusaidia kujifundisha kumtumainia ye ye peke yake. Katika nyakati hizi, tunaweza kuwa hatuelewi ni nini kinachoendelea na ni rahisi kuingia kwenye mtego wa kufikiria kwamba Mungu hatupendi. Hapo ndipo tunapohitaji kukumbuka Warumi 8:35-39, mistari inayosema kwamba hakuna chochote kitakachowea kututenganisha na upendo wa Mungu na kwamba sisi ni zaidi ya washindi katika Kristo Yesu. Kitu kizuri kabisa tunachowea kufanya tunapokuwa na shida ni kutamka kwa sauti na kusema, “Mungu, ninajua unanipenda, na ninaamini kwamba hili litafanya kazi kwa ajili ya mema kwangu.”

Wakati mwengine, Mungu hingojea kutukomboa mpaka tunafika mahali pa kufikiria kwamba amechelewa mpaka akapitwa na wakati. Unamkumbuka Lazaro? Alikuwa mgonjwa, lakini Yesu alingoja mpaka akafa kabla ya kwenda kumsaidia ye ye na familia yake. Martha alimwambia Yesu kwamba alikuwa amechelewa kabisa, lakini Yesu alikuwa anajua bila shaka yoyote kile alichokuwa akifanya, na Lazaro alirejeshewa uhai kwa njia iliyomtukuza Mungu kwa nguvu kuu. Huenda Mungu hatatenda kulingana na ratiba yetu, lakini hatawahi kuchelewa. Unapopatwa na shida maishani mwako, mkazie Mungu macho yako na uiweke imani yako kwa utendaji. Usiruhusu hofu na kuchanganyikiwa kuibe upendo wa Mungu kutoka kwako.

1 Yohana 4:18 ni andiko lililojaa nguvu nyingi ajabu: “Pendo lililo kamili huitupa nje hofu.” Nililitafakari andiko hilo tena na tena, nikijaribu kulielewa, na siku moja nikapokea ufunuo wake: pendo lililo kamili huitupa nje hofu, na Mungu ndiye pendo hilo lililo kamili. Ukifahamu jinsi upendo huo ulivyo mkamilifu kwako, hautaruhusu hofu ikutawale. Hata kama ukihisi hofu au woga, bado utaendelea

kupiga hatua za kwenda mbele na Mungu kwa sababu unajua kwamba yuko nawe daima.

Haiwezekani kuhofu kwamba utashindwa ikiwa unajua kwamba Mungu anakupenda. Unakuwa huru kujaribu vitu tofauti tofauti kwa sababu unajua kwamba upendo wa Mungu na kukubaliwa naye hakutegemei ubora wa matendo yako. Huwezi kushindwa ukimtegemea Mungu. Njia tu itakayokufanya ushindwe ni kujitegemea mwenyewe. Huenda ikatokea kwamba mambo hayatakuwa na hatima sawa na ile uliyokuwa ukiitarajia, lakini yataisha vyema ukiyaweka macho yako kwa Mungu. Ukiwa na usahamu thabiti kwamba Mungu anakupenda, hutaogopa kushindwa, kukataliwa, ufukara, yaliyopita, yajayo wala chochote kingine kile.

Upendo wa Mungu ni mkuu kiasi kwamba unafunika kila kitu. Unafikiri Mungu yule yule aliyeokuo na kukuweka huru atakufanya ujihisi kama mtu aliyeshindwa na asiyefaa? Atakuwacha bila msaada? Shetani ndiye adui wa nafsi zetu. Yeye ni mwizi na mwongo, lakini Yesu anataka tuwe na uzima tele na tuufurahie (tazama Yohana 10:10).

Katika tafsiri ya Biblia ya “THE AMPLIFIED”, 1 Yohana 4:18 inasema hivi: “Hakuna hofu katika pendo [woga haupo] lakini pendo lililokomaa [lisilokosa kitu, kamilifu] huondosha na kuitupa hofu nje na kufukuza tisho kabisa, kusiwe na tone moja iliyobaki. Maana hofu huja na wazo la adhabu, na [kwa hivyo] ye yote aliyeogopa hajafikia ukomavu kamili wa pendo [bado hajakua na kufikia ukamilifu wa pendo kamili].”

Punde tu baada ya Mungu kunisaidia kuelewa kwamba upendo wake huitupa nje hofu, ilinibidi niuweke usahamu huo kwenye vitendo. Gari letu lilikuwa lina shida. Ilionekana kwetu kana kwamba ni gia zake zilikuwa zinaenda kuharibika kabisa, na hatukuwa na pesa za kuweka gia zingine mpya. Kwa hivyo tulien��lea kuliendesha gari lile tukitarajia kwamba halitaharibika kabisa na kusambaratika.

Nilihisi Mungu akinitia moyo asubuhi moja na maneno haya. "Joyce, wewe tumia mda wa siku hii ukinipenda, na kupokea upendo wangu. Huna haja ya kufanya lolote lingine lile. Si lazima ujaribu kuwa mwanamke shupavu wa imani. Kile tu unachohitaji kufanya ni kudumu katika upendo wangu."

Kwa hivyo nikaanza kuimba, nikijitungia tenzi za kumwimbia Mungu na kuwa na wakati wa ajabu. Kisha ghafula, nikamsikia mume wangu akiwa kwenye kibanda cha kuegesha gari letu pale nyumbani – ikiwa ni dakika arobaini na tano tu baada ya kuondoka kwenda kazini. Akafungua mlango na kusema, "Sikuweza kuitoa gari kwenye gia ya kwanza. Lazima tuipeleke ikafanyiwe marekebisho."

Nikaufunga mlango na kuanza kucheka. Hicho si kitendo ambacho kwa kawaida ningekifanya, na hakikuwa kitu nilichoamua kufanya kwa hiari wakati huo. Kilitoka ndani yangu tu. Kwa sababu nilikuwa nikimruhusu Mungu anipende, nilikuwa na uwezo wa kucheka kati kati ya jambo gumu hivyo. Kudumu katika upendo wa Mungu hufungulia imani mlango itoke ndani yako badala ya hofu. Nilianza kucheka tu, na hiyo ilikuwa ni imani ikidhihirika. Nilicheka kwa sababu, kilindini mwa moyo wangu, nilijua hakika kwamba Mungu anatupenda na atakutana na hitaji letu hilo.

Ibrahimu naye alicheka kicheko cha imani. Mungu alipomjia na kumwambia kwamba atamzaa mtoto wa kiume, Ibrahimu alicheka! Aliuja kwamba hakukuwa na namna, kwa njia ya kawaida kulingana na asili ya kibinadamu, ambavyo ye ye na Sara wangeweza kupata mtoto, lakini alimwamini Mungu, na furaha yake ikabubujika na kufanyika kicheko.

Ninaamini kwamba kuenenda kwa namna kama hizo, kunamfungulia Mungu mlango ili atusaidie kwa njia za ajabu. Nani angeweza kufikiria kucheka anapopitia shida? Biblia inasema kwamba Mungu huketi mbinguni na kuwacheke adui zake (tazama Zaburi 2:2-4). Kama Mungu anaweza kufanya hivyo, basi tunaweza

kufanya hivyo pia. Maana liwe liwalo, Mungu anakupenda. Na ikiwa Mungu yuko upande wako, ni nani awezaye kukupinga na afaulu?



# 6



## UPENDO HUWAFIKIA WENGINE

*“Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.”*

- I YOHANA I 4:21

Wewe ni mtoto wa Mungu wa kipekee. Anakuambia hivyo katika Kumbukumbu la Torati 7:6. Unapokuja kujua na kuamini kwa kweli kwamba u spesheli kwake na kuishi na furaha na ujasiri unaotokana na ufahamu huo, utabadilisha ulimwengu unaokuzunguka kwa njia za baraka. Utaenda sokoni au kwenye duka kuu la kununua bidhaa ukiwa na tabasamu usoni, huku ukiwa unawaza, Ninapendwa. Kila kitu kiko sawa maishani mwangu. Ninaweza kuwabariki wengine na upendo wa Mungu ninao uhisi. Unaweza kufurahi popote uendapo, na furaha yako itawabariki wengine. Zaburi 100:2 inasema kwamba tunafaa “kumtumikia Bwana kwa furaha!”

Tunapoanza kufahamu jinsi tulivyo watu maalum katika mpango mkuu wa Mungu na nia yetu na mienendo yetu iwe matokeo ya ufunuo huo, tunaweza kushiriki habari za Kristo na kuuonyesha upendo wake kwa njia ambazo zitawavuta watu kwake. Upendo wa Mungu unaotiririka maishani mwako utakufanya mwelesi wa kuhisi mahitaji ya wengine na kukufanya uwahurumie. Upendo wake ndani yako utakuweka huru kutoka kwa hofu, na hutaogopa kuwafikia wengine kwa upendo. Hutaogopa kukataliwa, au kudanganywa kwa hila za

wanaojitafutia faida wao wenyewe; upendo wa Mungu ulio ndani yako utaona mahitaji wengine waliyo nayo na kujaribu kuyatimiza.

Mungu anataka umwamini anaposema kwamba atafanya mambo makuu zaidi kupitia kwako kwa sababu Yesu anaishi ndani yako. Mtumainie na uamini kwamba anataka kukutumia kuwapenda na kuwasaidia wengine. Kumbuka kwamba pendo kamilifu la Mungu huitupa hofu nje, kwa hivyo usiiruhusu hofu ikuzuie hata usiweze kuchukua hatua ya imani.

Siwezi hata kuanza kukuambia ni mara ngapi nimesimama kwenye “jabali la imani,” katika ukingo wa kufanya jambo la kuogofya, na ilikuwa ni kana kwamba Mungu alikuwa ananiambia, “Haya Joyce, haya. Nitafanya mambo makuu kupitia kwako. Haya, jaribu.” Kila mara nimechukua hatua ya imani na kuruka kuingia katikati ya jambo hilo, Mungu hajawahi kunipungukia.

Unajua ni kwa nini sisumbuki kuhusu kuchukua hatua hivyo na kushindwa? Kwa sababu ninajua Mungu ananipenda. Ananipenda, naye anajua ninampenda, na kupitia kwa neema yake nimeuotoa uhai wangu kwa ajili yake. Ukiwa umefanya hivyo, na unampenda Mungu na unajua anakupenda, basi hakuna shida ambayo huwezi kuishinda kupitia kwa Kristo.

Kama unatamani kwa kweli kuwasaidia wengine, Mungu atakusaidia kuwasaidia. Si lazima uwe na uweza mkubwa; unahitaji tu kujitolea kwa Mungu, naye atayatimiza mengine yote. Unaweza kuwa unahisi kwamba talanta zako ni za kawaida tu, lakini wakati mwingine kadri kitu kilivyo cha kawaida, ndivyo kilivyo cha nguvu.

Usiishi maisha yako kwa uchoyo ukitumia nguvu zako zote kwa mambo yanayo kuhusu wewe peke yako na kutimizwa kwa mahitaji yako. Mwambie Mungu unachohitaji au kile ungelipenda kuwa nacho halafu umtazame yeche, ili uweze kuwa makini kwa njia ambazo Roho Mtakatifu atakuongoza kuzifuata ili kuwafikia na kuwabariki wengine.

Kile utakachosaidia kimfanyikie mwengine, Mungu atahakikisha kikufanyikie. Unapokuwa na hitaji, uwe na nia ya “kupanda mbegu ya msaada” wala sio “kutimiziwa hitaji.” Hii inamaanisha kwamba unapowafikia wengine, Mungu huipokea kama mbegu uliyoipanda kwa ajili ya mavuno ya kile unachotamani kukiona maishani mwako.

Kila mtu anatamani kufaulu na kufanikiwa, lakini inatupasa kuelewa kufanikiwa kwa kweli ni nini. Ninapenda kuufafanua kuwa ni uwezo wa kutumia uwezo wa Mungu kukutana na kila hitaji unalokutana nalo. Upendo wa Mungu utakupa uwezo wa kuweka mahitaji ya wengine kwanza. Unafikiri na kuamini kwamba Mungu anakupenda vya kutosha kukuwezesha kuwafikia wengine kwa upendo, hata wale ambao si rahisi sana kuwapenda: wale waliojaa hasira na manung’uniko, wasiokuwa na moyo wa shukrani?

Huhitaji nidhamu nyangi kumpenda mtu anayekuonyesha upendo pia. Lakini lazima tuwe na neema ya Mungu ikituwezesha kuwapenda wale ambao si rahisi kuwapenda. Upendo wa Mungu ukiwa unatiririka maishani mwetu utaweza kufanya hivyo kwa sababu upendo wake hauna masharti. Tunaupokea bure na vivyo hivyo tunaweza kuutoa bure. Upendo haupungui neno wakati wowote, na haukat tamaa kuhusu watu. Inaweza kuchukua mwaka mmoja. Inaweza kuchukua miaka mitano. Inaweza kuchukua miaka ishirini na tano, lakin kuna thamani kuu katika kutokata tamaa. Ikiwa unapitia mda mgumu kuwa mvumilivu na kumpenda mtu ambaye si rahisi kumpenda, kumbuka nyakati zile ambazo Mungu ameendelea kukupenda akiwa anakungojea umruhusu akubadilishe.

1 Wakorintho sura ya 13 inatuambia kwamba upendo huvumilia, hufadhili na hunyenyeka. Hautafuti mambo yake, wala kukasirika haraka au kukwazwa kwa urahisi. Tabia hizo ndizo Yesu humimina juu yetu kupitia kwa upendo wake, nasi pia kwa upande wetu tunaweza kuudhihirisha upendo huo kwa kuwafanyia vivyo hivyo wale walioumizwa, watu waliopotea walio na njaa ya kupokea upendo wa Mungu katika maisha yao.

Mungu anakupenda, na anawapenda wote walio karibu nawe pia. Anawapenda, wawe wameokoka au bado hawaajaokoka, na anataka kikutumia kama mfereji wa kuwamiminia upendo wake.

Usiogope kuchukua hatua. Upendo wa Mungu unakuweka huru kutoka kwa hofu na hukumu ya adhabu, na amekupa uwezo wa kupenda. Kuwa na azimio thabiti la kushiriki upendo wa Mungu na wengine. Unaweza kuanza kwa njia rahisi ya kuwa mwema na mpole kwa wengine. Fanya uamuzi wa kuonyesha wema wa kirafiki na kuwa baraka kwa watu wengine popote uendapo.

Ukarimu ni njia moja ya kuonyesha upendo, hasa kwa mtu mpweke au aliyeshushwa moyo. Wakaribishe watu nyumbani kwako kushiriki chakula cha jioni. Karibisha wageni nyumbani kwako. Salimia watu kwa mkono na kutabasamu. Mkumbatie mtu mwingine au kumtia moyo. Toa msaada wa kimatendo, kama kumpa usafiri kwa gari lako mwingine ambaye labda gari lake linafanyiwa marekebisho. Msaidie mwajiriwa mpya kazini na uone kama unaweza kumsaidia kulifahamu jiji mnafanyia kazi vyema zaidi. Mungu ana kitu unachowenza kufanya. Huenda kisionekane kama kitu kikubwa au cha umuhimu mkuu kwako, lakini ni kitu muhimu kwake. Watu ni wa muhimu kwake Mungu!

Kuna watu ambaao ni wewe peke yako unaoweza kuwafikia. Muulize Mungu akuonyeshe njia za kuwafikia wengine na upendo wake, na atakufundisha jinsi ya kufanya hivyo.

# 7



## UPENDO WA MUNGU UTAKUBADILISHA

*“Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.”*

-I YOHANA 4:10

Mungu anatupenda, lakini sidhani kwamba wengi wetu hufahamu kwa kweli ukuu au kiasi cha upendo wake kwetu. Mungu amenionyesha, kuititia kwa masomo ya juhudhi kuu kuhusu mada hii, kwamba ikiwa kwa kweli tungalijua, kilindini mwa miyo yetu, ukuu wa upendo wake kwetu, basi matendo yetu yangalikuwa tofauti sana na yale tunayoyadhihirisha wakati mwingu.

Tafakari upendo wa Mungu kwako. Hilo ndilo litakalokubadilisha. Kama kuna jambo usilolipenda maishani mwako au katika tabia zako, basi kufahamu bila shaka na kuamini kwamba Mungu anakupenda unapomnongojea afanye kazi ndani yako kutakusaidia kuifurahia safari ya kubadilishwa kwako. Ukiendelea tu katika hali ya kusononekea kasoro na dosari zilizoko maishani mwako, huenda usibadilike hata kidogo. Kumbuka Mungu hufanya kazi kuititia kwa imani, na imani ya kweli hutuwezesha kuingia kwenye pumziko la Mungu (tazama Waebrania 4).

Inaonekana kwamba kuna watu wengi wasiokuwa na uhusiano mwema na wao wenyewe. Huwa hawajipendi tu; na inawezekana

kwamba hata wanajichukia. Ikiwa unashindana na hisia za kutojipenda, napenda nikukumbushe kwamba unaweza kuyachukia mabaya unayoyafanya, lakini ni lazima usijichukie kamwe. Yesu alikufa kwa ajili yako kwa sababu ya upendo wake mkuu kwako, na anataka ukipokee kipaji chake hiki cha thamani.

Biblia inasema, “Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo” (Mithali 23:7). Ukiwa na hisia mbaya kujihusu kila wakati, huku ukijikataa na kutojua jinsi ulivyo wa kipekee, utakosa amani na furaha ya Mungu, na nia na matendo yako yatadhihirisha hivyo. Na yote hayo ni kwa sababu bado hujashika na kuelewa moyoni mwako ukweli wa nguvu na wa kubadilisha maisha kwamba Mungu anakupenda zaidi ya vile unavyofahamu.

Mungu anataka uwe na wakati wa kuwa uweponi mwake kila siku. Hilo ndilo litakalokubadilisha. Usipomweka Mungu kwanza, basi utakuwa umemweka katika hali ambayo hataweza kukufanya kile alichokuwa amekusudia kukufanya. Ni mda ule unaokuwa na Mungu faraghani, ukimwonyesha upendo wako na ukimruhusu akupende, utakaokufanya uwe na nguvu, na ujasiri, na ukomae.

Watu wengi hutoa vijisababu na kamwe hawajitolei kuutumia mda unaohitajika kuujenga uhusiano mkuu na Mungu. Wangependa kuwa na uhusiano mwema naye, lakini hawaishi kwa nidhamu wala kuzikuza tabia nzuri kama kulisoma Neno kwa juhudhi na kuomba. Ikiwa una shida katika sehemu hii ya maisha yake, omba na kumwuliza Mungu akusaidie kuikuza tabia ya kuwa na wakati wa ushirika naye kila siku. Bila shaka kabisa, hicho ndicho kitu chema kabisa kwa vyote tunachowea kufanya!

Upendo wa Mungu utakubadilisha. Unapopata uzoefu wa upendo wake na kuufahamu nafsini mwako pamoja na kumakinika nao mara kwa mara kama kitu cha kawaiida, utapata matamanio yako yakibadiliika. Utatamani kuwa kama Yesu, yule akupendaye. Kujua na kuikuza tabia ya kiungu maishani mwetu yafaa kuwa mojawapo

wa mambo yaliyo na kipao mbele katika maisha yetu. Paulo alisema kwamba azimio lake hakika lilikuwa ni kumjua Kristo na nguvu za kufufuka kwake (tazama Wafilipi 3:10). Tafadhali tambua hapa kwamba Paulo alisema ilimbidi awe na azimio thabiti.

Nataka kikutia moyo umaanishe kuhusu uhusiano wako na Mungu. Unaweza kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu utakavyo; inategemea mda utakokuwa tayari kuwekeza kwa uhusiano huo.

Biblia inasema kwamba sisi ni wawakilishi wa kibinagsi wa Mungu na kwamba Mungu anausihi ulimwengu kupitia kwetu (tazama 2 Wakorintho 5:20). Andiko hilo kila wakati hugusa moyo wangu kwa njia kuu na hunifanya kufahamu upya jinsi ilivyo muhimu kwetu kwamba tuufuate mwongozo wa Roho wa Mungu anapofanya kazi ndani yetu, akitubadilisha na kutuunda kwa ajili ya kutimiza kusudi la Mungu. Upendo wa Mungu humiminwa miyoni mwetu na Roho Mtakatifu (tazama Warumi 5:5). Upokee, ufurahie, na wacha ukubadilishe!

# PATA UZOEFU WA MAISHA MAPYA



Kama hujawahi kumkaribisha Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako, nakualika ufanye hivyo sasa. Ombo ombi hili na moyo ulio wazi na wa kumaanisha na uanze kuyafurahia maisha mapya ndani ya Kristo ambayo Mungu ameyatayarisha kwa ajili yako.

*Mungu Baba, ninaamini Yesu Kristo ni Mwanao, Mwokozi wa ulimwengu. Ninaamini alinifia msalabani, na kuzibeba dhambi zangu zote. Alifufuka kutoka kwa wafu na kwa kufanya hivyo, akayashinda mauti pamoja na kaburi. Ninaamini Yesu yu hai sasa hivi na ameketi kwenye mkono wako wa kuume.*

*Ninakuhitaji Yesu. Nisamehe dhambi zangu, niokoe, njoo uishi ndani yangu. Ninataka kuzaliwa mara ya pili. Ninataka kukuishia. Asante kwa kuniokoa na kunisaidia niishi maisha mapya kwa ajili yako.*

Sasa amini kwamba Yesu anaishi moyoni mwako. Amini kwamba umesamehewa, umefanywa haki kupitia kwa damu ya Yesu, na kwamba utaenda mbinguni siku moja.

Pata kanisa zuri la kwenda, mahali ambapo wanafundisha Neno la Mungu na unaweza kukua katika uhusiano wako na Kristo. Tunabadilika kupitia kwa nguvu za upendo wa Mungu na utendaji wa Neno lake maishani mwetu, kwa hivyo ni muhimu kwetu kuufahamu ukweli wa Neno la Mungu. Yohana 8:31-32 inasema, “Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.”

Nakusihii ulichukue Neno la Mungu na kulipanda ndani kabisa moyoni mwako, na kulingana na 2 Wakorintho 3:18, unapoliangalia Neno, utabadalishwa na kufananishwa na mfano wa Yesu Kristo.

Tafadhalii niandikie barua uniambie umemkaribisha Yesu

maishani mwako, na uulize kupewa bila malipo kitabu kuhusu jinsi  
ya kuanza maisha yako mapya ndani ya Kristo.

Na upendo,  
*Joyce*

# OMBI KWA AJILI YA KUOKOKA



Mungu anakupenda, na anataka kuwa na uhusiano wa kibinagsi nawe. Ikiwa hujampokea Kristo kama mwokozi wako, unaweza kufanya hivyo hivi sasa. Fungua moyo wako kwake na uombe ombi hili.

*“Baba, najua kwamba nimetenda dhambi mbele zako. Naomba unisamehe. Nioshe niwe safi. Naahidi kumtumaini Yesu Mwanaao. Naamini kwamba alinifia- Alijichukulia dhambi yangu alipokufa msalabani. Naamini kwamba alifufuliwa kutoka kwa mauti. Nayasalimisha maisha yangu kwa Yesu hivi sasa.*

*Asante Baba, kwa kipawa chako cha msamaha wa dhambi na uzima wa milele. Tafadhali niwezeshe kukuishia, katika jina la Yesu, Amina.”*

Kwa vile umeomba kutoka moyoni mwako, Mungu amekupokea, amekuisha na kukuweka huru kutokana na utumwa wa mauti ya kiroho. Chukua muda usome na kuelewa maandiko haya na umuulize Mungu akunenee unapotembea naye katika safari hii ya maisha mapya.

Yohana 3:16

1Wakorintho 15:3-4

Waefeso 1:4

Waefeso 2:8-9

1Yohana 1:9

1 Yohana 4:14-15

1 Yohana 5:1

1 Yohana 5:12-13

Muombe Munguakuwezeshe kupata kanisa ambalo linaamini mafunzo ya bibilia ili uweze kuhimizwa kukua katika uhusiano wako na Kristo. Mungu yuko nawe kila mara. Atakuongoza siku baada ya siku na kukufunza jinsi ya kuishi maisha ya utele aliyonayo kwa ajili yako.

# KUHUSU MWANDISHI



JOYCE MEYER ni mmoja kati ya viongozi mashuhuri ulimwenguni katika kufundisha jinsi ya kuweka kweli za Biblia kwenye vitendo. Akiwa mwandishi mashuhuri kwa mujibu wa gazeti la New York Times, vitabu vyake vimesaidia mamilioni ya watu kupata tumaini na urejesho kupitia kwa Yesu Kristo. Kupitia kwa huduma ya Joyce Meyer Ministries, ye ye hutoa mafundisho kuhusu mada kadhaa, mafundisho hayo yakiwa hasa yamelenga fahamu, mdomo, hisia tawala na nia. Namna yake ya kuwasiliana bila kuficha chochote humruhusu kushiriki kwa uwazi na kwa njia ya kimatendo yale aliyoyapitia, ili wengine waweze kuzitumia kweli alizojifundisha katika maisha yao. Joyce ameandika karibu vitabu 100 ambavyo vimetafsiriwa kwa lugha 100. Yeye huongoza karibu kongamano kumi na mbili nchini na kimataifa kila mwaka, akiwfundisha watu kuyafurahia maisha yao ya kila siku. Kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita, kongamano lake la wanawake la kila mwaka limewavutia na kuhudhuriwa na zaidi ya wanawake 200,000 kutoka kote ulimwenguni. Ashiki ya Joyce ya kuwasaidia watu wanaoumia na kupitia magumu ndio msingi wa *Hand of Hope*, kitengo cha kazi ya umisheni cha huduma ya Joyce Meyer Ministries, kinachotoa msaada wa kuwafikia wengine ulimwenguni kote, pamoja na anakoishi, mjini St. Louis.



## Gundua Karama ya Mungu Kwako: Upendo Usio na Masharti!

Kila chembechembe ya nguvu za Mungu na upendo wake inaweza kupatikana kwako – leo! Na wewe si mtu mmoja tu kati kati ya umati mkubwa wa watu. Mungu anakupenda kana kwamba ni wewe peke yako uishiye duniani. Shida ni kwamba, jinsi ilivyo na watu wengi, huenda hujauelewa ukweli huu... au ikiwa unaufahamu akilini, labda huuhisi moyoni mwako. Sasa waweza. Ujumbe wa nguvu ulio kwenye kitabu hiki cha kuvuvia utakuonyesha:

- Jinsi ya kuutambua upendo wa Mungu ndani yako.
- Unavyoweza kushinda wasiwasi kuhusu kama u mwema vyakutoisha kwa Mungu.
- Jinsi unavyoweza kuwa na uzoefu wa ufunuo wa ajabu wa upendo wa Mungu.
- Jinsi ya kumpata Mungu hata unapopitia nyakati za uchungu maishani.
- Jinsi upendo wa Mungu utakavyokubadilisha milele.

Akishiriki vidokezo na ufunuo uliobadilisha maisha yake mwenyewe, Joyce Meyer anakuletea maandiko na maneno mengine ya hekima yanayoweza kuifungua dirisha ya upendo wa Mungu...na kuiruhusu nuru ya upendo huo ikuangazie, wewe kama mtu binafsi!

WAAMBIE NINAWAPENDA NA JOYCE MEYER



JOYCE MEYER  
MINISTRIES®

P.O. Box 5, Cape Town, 8000, South Africa